8:1-13:31 MAREKEBISHO YA NEHEMIA

Masomo ya kwanza ya sheria (8:1-18)

Ukuta ulimalizika siku ya 25 ya mwezi wa sita (yaani muda wa ujenzi ulikuwa siku 52, taz.6:15). Sikukuu ya Israeli ya katikati ya mwaka iliadhimishwa katika mwezi wa saba (Law 23:24,27,34), na hiyo ilikuwa nafasi nzuri ya kuwakutanisha watu wote ili kusherehekea pia kumalizika kwa ukuta uliojengwa upya (taz.7:73; 8:1). (Wakati ule ule wa mwaka ulikuwa umechaguliwa kwa kuweka wakfu madhabahu iliyojengwa upya zaidi ya miaka 90 ya awali; taz.Ezra 3:1-6).

Kufuatana na maombi ya watu, Ezra aliyesaidiwa na baadhi ya Walawi, alisoma sheria na kuieleza kwa watu waliokutana. Inaonekana kwamba sheria haikusomwa kwa muda mrefu sana, kwa hiyo watu walisikiliza kwa uangalifu sana (8:1-8). Walipogundua jinsi maisha yao yalivyokuwa mbali na sheria hiyo, walijaa huzuni. Nehemia aliogopa kwamba mambo yale aliyoyakusudia kuwa sikukuu ya furaha na karamu kubwa yangegeuka kuwa wakati wa huzuni na maombolezo (9-12).

Siku ya pili yake viongozi wa Israeli walirudi tena ili wasikilize zaidi ya sheria ya Mungu (13). Matokeo ya mambo hayo yalikuwa sherehe kubwa ya taifa zima ya sikukuu ya Vibanda. Wakati wa sikukuu hiyo watu waliishi katika vibanda vya matawi ya miti na makuti, wakiwakumbuka mababu zao jinsi walivyoishi katika vibanda wakati wa safari yao ya jangwani walipotoka Misri (14-18; taz.Law 23:33-43).

Maungamo ya Waisraeli na kiapo chao cha kutii (9:1-10:39)

Siku mbili baada ya kumaliza sikukuu ya Vibanda (iliyokuwa tangu siku ya 15 hadi ya 22 ya mwezi ule, taz.8:18; Law 23:34), watu walikutana tena kwa kusomewa sheria. Wakati huo baada ya kusomewa, ulifuata wakati wa kukiri dhambi na kumwabudu Mungu. Ibada hiyo iliongozwa na Walawi (9:1-5).

Ibada ilianza kwa kumtukuza Mungu mkuu aliye Mwumbaji, na kwa kumsifu kwa sababu ya kumchagua Ibrahimu na kufanya naye agano lake (6-8). Mungu siku zote alikuwa mwaminifu kwa watu wake wa Israeli, wakati wa shida zao huko Misri na hata katika safari kubwa ya jangwani (9-15). Hata walipomwasi, aliwasamehe na kuwaleta katika nchi ya ahadi yake (16-25). Wakaendelea kuasi, naye Mungu akaendelea kuwasamehe. Lakini waliendelea na ukaidi wao, hata mwisho, baada ya kushindwa na kunyanyaswa mara nyingi na maadui zao, walipelekwa kifungoni katika nchi za kigeni, kusudi Mungu aweze kuwanyenyekeza na kuwasababisha watubu (26-31). Ingawa wakati huo walikuwa wamerudi katika nchi yao, bado walikuwa chini ya utawala wa wageni. Walikubali kwamba mambo hayo yalikuwa adhabu ya haki kwa ajili ya dhambi zao, kwa sababu walikuwa wakiasi agano la Mungu (32-37).

Baada ya kukiri makosa yao, watu walitoa ahadi ya agano kuwa waaminifu kwa Mungu. Walithibitisha ahadi yao kwa kiapo kilichoandikwa na kutiliwa sahihi na viongozi wao kwa niaba yao (38). Nehemia alikuwa wa kwanza wa kutia sahihi (10:1), akifuatwa na makuhani (2-8), Walawi (9-13) na viongozi wa kiraia (14-27). Watu wote waliapishwa juu ya maandiko ya agano hilo kuwa waaminifu kwa sheria ya Mungu (28-29).

Mambo muhimu zaidi yaliyotajwa katika maandiko haya yalihusu ndoa za mchanganyiko (30, taz.Kut 34:15-16); siku ya Sabato na mwaka wa Sabato(31,taz.Kut20:8-10;23:10-ll;Kum 15:1-2); kodi ya hekalu (32, taz.Kut 30:11-16); mahitaji kwa ajili ya hekalu na huduma zake (33-34); sadaka za malimbuko ya nafaka na wazaliwa wa kwanza wa wanyama (35-36, taz.Hes 18:13-18) na zaka (yaani utoaji wa sehemu ya kumi ya mapato, 37-39; taz.Hes 18:21-28).

Orodha za wenyeji wa Yerusalemu (11:1-12:26)

Watu wengi zaidi waliorudi kutoka kifungoni waliishi katika nchi iliyozunguka Yerusalemu kuliko katika jiji lenyewe. Kwa hiyo wenyeji wa jijini walikuwa wachache, na mikakati ikafanyika ili kupata wenyeji zaidi jijini. Katika mpango huo kila mtu wa kumi wa wenyeji walioishi katika maeneo ya nchini alipaswa kuhamia Yerusalemu, na hivyo jiji la Yerusalemu liliimarishwa. Zaidi ya hayo, kulikuwa na kundi kubwa la watu waliokuja kwa hiari yao na waishi jijini (11:1-2).

Hapa tunapata orodha ya wakuu wa jamii mbalimbali waliokuwa wamerudi pamoja na Zerubabeli. (Wazao wa jamii zile wangalikuwa wenyeji hasa wa Yerusalemu wakati ambapo mpango mpya wa uhamiaji wa jijini uliwekwa.) Licha ya watu wale wa makabila ya Yuda na Benyamini (3-9), wengi wao wanaonekana kuwa ni makuhani, Walawi au watumishi wa hekaluni (10-21; taz. maelezo ya 1 Nya 9:1-34, ambapo orodha iyo hiyo imeandikwa yenye mabadiliko na nyongeza chache tu). Mipango

mingine ilifanywa kwa kuangalia kazi za Walawi, kuhusu waimbaji wa hekaluni na kumpata mjumbe wa Kiyahudi katika mahakama ya mfalme wa Uajemi (22-24). Kisha orodha nyingine inafuata yenye majina ya miji iliyohamiwa upya na watu. Miji hiyo ilikuwa katika maeneo ya Yuda na Benyamini ya hapo awali (25-36).

Orodha za makuhani na Walawi (12:1-26)

Orodha nyingine ina majina ya makuhani na Walawi waliorudi pamoja na Zerubabeli na Yoshua (12:1-9). (Ezra aliyetajwa katika orodha hiyo siyo yule anayejulikana sana.) Baada ya kuwaorodhesha watu wa vizazi sita vya Yoshua (10-11), mwandishi anarudia kuorodhesha vichwa vya nyumba nyingine za makuhani wa asili (12-21).

Licha ya kushughulika na familia za makuhani, maelezo pia yalihusu watumishi wa kawaida wa hekaluni. Maelezo mengine yalihusu hata mambo ya baada ya wakati wa Nehemia (22-26).

Kuzindua ukuta wa jiji (12:27-13:3)

Habari zinaendelea tena pale zilipoachwa kwanza katika 10:39. Baada ya kusoma sheria, kusherehekea sikukuu ya Vibanda na kiapo cha watu kuhusu uaminifu wao kwa agano, ukuta ulizinduliwa (au kufunguliwa rasmi). Makuhani, Walawi, waimbaji na wenyeji wengine wenye heshima walishiriki katika sherehe hiyo (27-30). Watu walikutana sehemu moja karibu na ukuta upande mmoja wa jiji. Kisha wakagawanyika kuwa makundi mawili wakaanza kwenda kila upande kuzunguka ukuta wote. Kundi moja liliongozwa na Ezra (31-37) na lingine liliongozwa na Nehemia (38-39). Makundi mawili yakakutana tena upande mwingine wa jiji karibu na hekalu watu walipounganika kwa kutoa sadaka na kumtukuza Mungu kwa furaha kubwa (40-43).

Hatimaye maafisa wakawekwa ili waangalie michango na matumizi ya fedha na vitu vingine ambavyo watu walivileta hekaluni. Waisraeli wote walitoa sehemu ya kumi ya mapato yao wakaiweka katika fungu hilo la jumla. Kutoka huko vitu vile vikagawiwa kwa Walawi waliowasaidia makuhani na kushughulika na nyimbo na muziki hekaluni. Walawi tena walitoa sehemu ya kumi ya mapato yao kuwa posho ya makuhani (44-47). Masomo mengine ya sheria yaliwaonya watu kwamba walipaswa kutunza utakatifu wa hekalu. Wapagani au watu wa mataifa hawakuruhusiwa kuingia hekaluni (13:1-3).

Marekebisho ya Nehemia ya baadaye (13:4-31)

Baada ya miaka 12 ya kuwa liwali wa Yerusalemu, Nehemia alimrudia mfalme wa Uajemi kwa muda (taz.5:14; 13:6). Wakati ule ambao Nehemia hakuwepo Yerusalemu, dini ya Wayahudi ilirudi nyuma, na maadui zao wa zamani, yaani San-balati na Tobia waliweza kupata nafasi ya ushawishi wao tena Yerusalemu. Kuhani mkuu, Eliashibu, alistahili kulaumiwa zaidi katika mambo hayo. Alimruhusu mtu wa familia ya kuhani mkuu kumwoa binti wa San-balati (taz.mst. 28), pia alimruhusu Tobia aishi katika chumba cha hekaluni. Jambo lile lilikuwa kinyume kabisa cha sheria ambayo Nehemia alijaribu kuitekeleza vizuri, kwa sababu Tobia alikuwa Mwamoni (taz.4:3; 13:1). Nehemia aliporudi Yerusalemu alirekebisha mambo hayo mara moja (4-9).

Nehemia pia aligundua kwamba watu walikuwa wamevunja ahadi mojawapo ya maana sana ya agano waliyokuwa wametoa wakati wa kuweka wakfu ukuta wa jiji. Hawakutoa zaka zao, na matokeo yake, Walawi walipaswa kuacha huduma yao hekaluni na kwenda mashambani kwao ili kutafuta riziki zao (10-14; taz. 10:35-39).

Pia watu walifanya kazi na biashara siku ya Sabato, na hivyo walivunja sheria nyingine ya ahadi ya agano (15-18; taz. 10:31). Kwa haraka Nehemia alifikisha mambo hayo katika mwisho wake. Kwa njia ya kufunga milango ya jiji siku ya Sabato, aliwazuia watu waliotaka kuleta bidhaa zao jijini. Pia aliwazuia wasiuze nje ya malango au kungoja huko wakijiandaa kuuza mara baada ya kupita Sabato (19-22).

Siku za Ezra watu walikuwa wameapa kwamba wawaondoe wake zao wa kigeni, na kweli walifanya hivyo (Ezra 10:19,44). Wakati huo desturi ile mbaya ilienea tena, nayo ilitishia kuharibu dini ya Waisraeli. Kwa ushujaa ule uliokuwa tabia ya Nehemia, alirekebisha hali hiyo (23-29). Hakuna shaka lo lote kwamba yeye, zaidi ya mtu ye yote, aliwasaidia watu wa wakati ule kutengeneza maisha yao katika msingi wa dini ya kweli kadiri ya sheria ya Mungu (30-31).